HAZINA YA MSAADA YA COVID-19 YA WASHINGTON KWA MHAMIAJI

Zana ya Ujumbe

Inasaidiwa na kufadhiliwa na Idara ya Jamii na Huduma ya Afya ya jimbo la Washington.

Zana ya ujumbe kuhusu hazina ya msaada ya COVID-19 kwa mhamiaji

Muhtasari

Karibu! Asante kwa kazi yako ya kusaidia kueneza habari kuhusu Hazina ya Msaada ya COVID-19 kwa mhamiaji.Lengo la zana hii ya ujumbe ni kukusaidia wewe katika juhudi zako za kuwafikia wahamiaji wa Washington.Na huu mpango wako wa kuwafikia watu, tunatumai kwamba habari kuhusu hazina hii itawafikia watu wengi iwezekanavyo, na watahisi wametiwa moyo kutuma maombi. Tunakushukuru kwa kujitolea kwako kuhakikisha kuwa majirani zetu wahamiaji, wengi iwezekanavyo wanauwezo wa kupata raslimali zinazohitajika.

Zana hii ya ujumbe ni ya nani?

Zana hii ni ya mashirika ya jamii, viongozi,na wanachama wa jamii kutumia kueneza habari kuhusu Hazina ya Msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji, wasaidie watu kuelewa inahusu nini na inatumikaje, kisha wahimize watume maombi.

Jinsi ya kutumia zana hii

Tumia mfano wa ujumbe ulioko hapo chini ili kutuma habari ya kuunga mkono kupitia kituo chako cha kibinafsi au cha shirika.Bila shaka, Tafadhali ibinafsishe iwe sauti na toni yako mwenyewe.

Ujumbe na orodha ya maswali na majibu kuhusu suala fulani kwa watumiaji wa mtandao

Muhtasari wa ujumbe

Ujumbe wa hadhi ya juu

Msaada wa dharura wa COVID-19 —na wahamiaji kwa wahamiaji.

Kaulimbiu

Wahamiaji wanaotunzana

Ujumbe mfupi wa kushawishi

Kama wahamiaji,tumefanya Washington kuwa nyumbani kwetu. Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia wakati mgumu kwa sababu ya COVID-19, na hujafuzu kupata msaada wa serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira,hazina hii ni kwa ajili yako. **Tuma maombi ya kupata Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji na upate dola elfu moja ambayo utapata mara moja na utatumiwa moja kwa moja (unaweza pata hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba).** Maelezo yako kamwe hayatasambazwa kwa hiari kwa serikali au ICE, na sheria ya malipo ya umma haitatumika katika hazina hii.Unawezapata usaidizi wa kutuma maombi kwa lugha kadhaa.Siku ya mwisho ya kutuma maombi ni Disemba tarehe 6.

Ujumbe mrefu wa kushawishi

Katika jimbo la Washington, wahamiaji siku zote wamekuwa majirani na wafanyakazi wa huduma muhimu. Tunasaidia uchumi kuwa imara, Tunatoa mchango katika jamii yetu, na tunatunza familia zetu.

Wakati huu wa tandavu ya COVID-19, tumekuwa katika hatari kubwa zaidi ya kupata virusi, kupoteza kazi, au kuhitaji kusaidia watu wa familia zetu kwa njia mpya.Lakini serikali ya ugatuzi kimakusudi iliwacha mamilioni yetu nje ya msaada wa kifedha uliohitajika sana, Kutokana na hali ya uhamiaji.

Hili ni kosa. Sisi sote ambao tunaita Washington nyumbani tunastahili kupata msaada ili tuweze kujimudu wakati huu mgumu.

Hii ndio sababu sisi kama mashirika yanayoongozwa na wahamiaji tulishirikiana na afisi ya Gavana kuanzisha Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji. Mwaka huu, tutasambaza dola millioni arobaini za hazina ya CARES zilizotengewa jimbo la Washington kusaidia wahamiaji wa Washington ambao hawafuzu kupata msaada wowote wa serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira kwa sababu ya hali yake ya uhamiaji.

Unaweza tuma maombi ili upate dola elfu moja ambayo utapata wakati mmoja na utatumiwa moja kwa moja (unaweza pata hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba). Maelezo yako kamwe hayatasambazwa kwa hiari kwa serikali au ICE, na sheria ya malipo ya umma haitatumika katika hazina hii.Unawezapata usaidizi wa kutuma maombi kwa lugha kadhaa.Siku ya mwisho ya kutuma ombi ni Disemba tarehe 6.

Tutafanikiwa wakati huu—kwa sababu sisi ni wahamiaji tunaotunzana.

Jinsi ya kuzungumza kuhusu hazina hii

Ni muhimu kuzungumza kuhusu hazina hii kwa njia ambayo ni ya kweli na sahihi na yenye toni ya kuhimiza. Unapozungumza kuhusu hazina hii, jaribu kuifanya:

- **Chanya na yenye matumaini**—tunafaa kutambua ukweli wa tandavu ya COVID-19, lakini tusambaze ujumbe wa matumaini na ujasiri kuhusu hazina hii.
- **uhalisia**—hazina hii haitasuluhisha kabisa matatizo ya watu, na kwa sababu ufadhili ni mdogo, sio kila mtu ambaye atatuma maombi atapata pesa. Tusitoe ahadi nyingi tunapozungumza kuhusu hazina hii.
- **kuhamasisha**—hazina hii ni ushindi uliopiganiwa sana kwa sababu ya wahamiaji wa Washington. Ni mashirika ya wahamiaji ndio yalishinikiza kuundwa kwa hazina hii na kufanya kazi na afisi ya Gavana na Idara ya jamii na huduma ya afya ili kufanya ifaulu. Tunapaswa kuzungumzia hazina hii kama wahamiaji wanaotunzana, sio hisani ya serikali.

Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji ni nini?

Ujumbe muhimu

Sisi sote tunaadhirika na COVID-19, lakini watu wengi wa Washington hawafuzu kupata msaada wowote wa serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira kwa sababu ya hali yake ya uhamiaji. Kwa hivyo Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji ilitengwa kusaidia wahamiaji. Unaweza tuma maombi ili upate dola elfu moja ambayo utapata wakati mmoja na utatumiwa moja kwa moja, unawezapata hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba.

Jumbe za ziada

- Baada ya COVID-19 kutuwahi, serikali ya ugatuzi ilituma dola elfu moja mia mbili kama malipo ya msaada kusaidia watu wengi hapa Marekani —na watu wengi wanauwezo wa kupata bima kwa wasiokuwa na ajira pia. Lakini wengi wetu tuliwachwa nje kwa sababu ya hali zetu za uhamiaji.
- Kwa kujibu, muungano wa mashirika ya wahamiaji waliomba serikali ya jimbo la Washington kuunda hazina ya msaada haswa kwa wahamiaji. Kwa kuelewa umuhimu wa usaidizi, Gavana alitenga hazina ya dola millioni arobaini kusimamiwa na mashirika

yasiyokuwa ya kiserikali kwa usaidizi kutoka kwa jimbo la Washington idara ya jamii na huduma ya afya.

Kwa nini Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iliundwa?

Ujumbe muhimu

Kama wahamiaji, tumekuwa baadhi ya watu walioathiriwa zaidi na tandavu ya COVID-19. Ilikuiweka jamii yetu salama na yenye afya nzuri, tunahitaji kusaidiana sasa hivi.ndiyo maana mashirika ya wahamiaji yalifanya kazi na jimbo la Washington ili kupata ufadhili kwa sababu ya wahamiaji ambao hawakuwa na uwezo wa kupata msaada wa serikali.

Ujumbe wa ziada

- Washington ni nyumbani kwa maelfu ya wahamiaji. Sisi ni wafanyakazi wa huduma muhimu hapa Washington katika viwanda kubwa zaidi, kama vile kilimo na ujenzi—na tunatoa mchango wa zaidi ya dola bilioni kwa serikali,jimbo, na ushuru wa mitaa kila mwaka. Sisi ni majirani, marafiki, wafanyakazi wenza, na wanafamilia.
- Jamii zetu ni baadhi ya zile zilizoathiriwa sana na COVID-19. Wengi wetu tumepoteza kazi, wengine wanaenda kila siku kwa makazi yanayowafanya kuwemo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi, na wengine wanawatunza wanafamilia walioko nyumbani kwa sababu ya virusi. Wengine wetu wanaomboleza kupoteza wapendwa wao.
- Wakati kila mmoja anajua kwamba sisi ni wafanyakazi wanaotoa huduma muhimu na majirani, hatujakuwa tukishughulikiwa hivyo: hazina ya msaada ya serikali kimakusudi ilitenga mamilioni yetu kwa misingi ya hali zetu za uhamiaji.
- Hii ndio sababu mashirika ya jamii yanayoongozwa na wahamiaji wakishirikiana na afisi ya Gavana, idara ya jamii na Huduma ya afya ya Washington, na wakfu wa sheria ya Washington waliunda hazina hii. Sote tunaoita jimbo hili nyumbani tunastahili kupata msaada tunaohitaji ili tujimudu wakati huu mgumu.

Ninaweza pokea kiasi gani kupitia hazina hii?

Ujumbe muhimu

Unaweza tuma ombi ili upate malipo ya wakati mmoja ya dola elfu moja kwa kila mtu utakayotumiwa moja kwa moja, malipo ya juu zaidi ni dola elfu tatu kwa kila nyumba. Unaweza pokea pesa hizi kama hundi au kadi ya zawad (Visa)

Ni nani anawezatuma maombi?

Ujumbe muhimu

Ili kutuma maombi ya hazina ya msaada, ni lazima:

- Uwe unaishi katika jimbo la Washington
- Uwe na angalau umri wa miaka kumi na nane
- Uwe umeathirika kwa kiasi kikubwa na tandavu hii (kama vile kupoteza kazi, uwe umeambukizwa na virusi, au kumtunza mtu wa familia aliyeambukizwa na virusi)
- Usiwe unafaa kupata dola za msaada za serikali au pesa za bima kwa asiyekuwa na kazi kwa sababu ya hali ya uhamiaji

Ujumbe wa ziada

- Maombi yatakubaliwa kwa msingi wa atakayetuma maombi wa kwanza ndiye atakayehudumiwa wa kwanza kwa sababu jumla ya hazina ya msaada ni mdogo. Tutawapa kipaumbele wale wanaohitaji msaada zaidi.

Je! watu wengi kutoka nyumba yangu wanaweza tuma maombi?

Ujumbe muhimu

Ndio, kila mtu anayetoka kwa nyumba yako na ana miaka kumi na nane au zaidi anastahiki kupata msaada wa hazina na anaweza tuma maombi. Kila mtu ni lazima ajaze fomu yake binafsi ya kutuma maombi. Ufadhili hautatolewa kwa zaidi ya watu watatu katika kila nyumba (malipo ya juu zaidi ni dola elfu tatu kwa kila nyumba)

Nitatuma maombi vipi?

Ujumbe muhimu

Unaweza tuma maombi kwa kutumia mtandao, kupitia simu, au kwa kutuma barua.
Njia zote tatu zinapatikana kwa Kiswahili. Siku ya mwisho ya kutuma maombi ni Disemba tarehe 6.

- Tovuti: www.immigrantreliefwa.org
- Simu: 1-844-724-3737 (Jumatatu-Ijumaa saa tatu asubuhi hadi saa tatu usiku
- Barua: Tembelea tovuti ili uchapishe fomu ya kutuma maombi

Ujumbe wa ziada

- Kabla ya kutuma maombi, utahitajika kuwa na stakabadhi fulani zitakazo kutambulisha na kuonyesha unaishi katika jimbo la Washington. Kwa mfano, unaweza kutoa nakala ya

kitambulisho cha jimbo/serikali, leseni ya udereva, au bili ya matumizi iliyo na jina lako na anwani yako. Tazama orodha kamili ya stakabadhi zinazokubalika.

- Tuma maombi mtandaoni kupitia tovuti ya www.immigrantreliefwa.org. Fomu ya maombi inapatikana katika lugha kadhaa:
    - Kichina
    - Kiingereza
    - Kifaransa
    - Kigarifuna
    - Kihindi
    - KiKorea
    - Kisomali
    - Kihispania
    - Swahili
    - KiTagalogi/Kifilipino
    - Kivietinamu
- Ikiwa una maswali yoyote, piga simu kwa Hazina ya mshikamano wa wahamiaji ya Washington (WAISN) piga simu kwa 1-844-724-3737. Usaidizi unapatikana kila siku kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa tatu usiku, na watu watakuwepo kuzungumza kwa lugha kadhaa.
- Baada ya kutuma maombi, utakuwa ukipata sasisho kuhusu maombi yako kupitia barua pepe au arafa kwa simu. Utafahamishwa ikiwa maombi yako yatakubaliwa ndani ya wiki tatu baada ya kutuma maombi. Ikiwa maombi yako yatakubaliwa, utapokea malipo ndani ya wiki mbili baada ya maombi kukubaliwa.
- Hazina yetu ni ndogo, kwa hivyo si kila mtu anayetuma maombi ataweza kupata msaada wakati huu.

Hizi ndizo stakabadhi unazoweza kutumia unapotuma maombi yako kudhibitisha utambulisho wako na kuwa unaishi katika jimbo la Washington.Hakikisha kuwa una nakala safi inayoonekana ya mojawapo:

- Bidhaa moja kutoka kwa orodhaa A, au
- Bidhaa moja kutoka kwa orodha zote B na C

Orodha A: Stakabadhi za makazi na kitambulisho	**Orodha B: stakabadhi ya kujitambulisha**	**Orodha C: Stakabadhi ya makazi**

● Kadi ya Kitambulisho cha jimbo la Washington linaloonyesha jina kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Leseni ya udereva ya Washington inayoonyesha jina kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Kadi ya kitambulisho ya sasa kutoka kwa shule ilioko katika jimbo la Washington ● Bili yoyote inayoonyesha jina kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Bili ya simu au mtandao inayoonyesha jina kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Taarifa ya bima inayoonyesha jina lako kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Taarifa ya benki inayoonyesha jina lako kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Taarifa ya kurudisha kodi ya mwaka wa 2019 inayoonyesha jina lako kamili na anwani ya jimbo la Washington ● Barua ya malipo kutoka kwa mwajiri inayoonyesha jina lako kamili na anwani ya unakokaa katika jimbo la Washington ● Risiti ya kodi ya nyumba inayoonyesha jina lako kamili na anwani ya jimbo la Washington	● Kadi ya kitambulisho cha mwanafunzi kutoka kwa shule yoyote ● Pasipoti kutoka nchi yoyote ● Kadi ya ubalozi ● Cheti cha kuzaliwa ● Leseni ya udereva ya kimataifa ● Kadi ya Metro iliyo na picha	● Barua iliyowekwa sahihi na tarehe na itaje jina kamili na nambari ya simu ya anayeandika barua kutoka kwa taasisi zifuatazo: ○ Mpangishaji akitambua kuwa wewe ni mkazi wa WA ○ Mwakilishi kutoka mahali unapoabudia akitambua kuwa wewe ni mkazi wa WA

Je habari yangu iko salama?

Ujumbe muhimu

Maelezo yako ya kibinafsi hayatasambazwa kwa hiari kwa serikall, ICE, watekelezaji sheria, Mpangishaji wako, mwajiri wako, au mtu yeyote. Maelezo yote yamehifadhiwa kwa njia salama kwa mfumo fiche kwa hivyo hayawezi kufikiwa.

Ujumbe wa ziada

- Kulingana na kandarasi yetu na idara ya jamii na huduma za afya ya jimbo la Washington, Wale ambao wanauwezo wa kuona maelezo yako ya kibinafsi ni wadhamini wasaidizi,(shirika la jamii linalosimamia hazina) kituo cha Fair Work, na chama cha mikopo cha Seattle (linalosambaza pesa).Hatutasambaza habari yako kwa mtu yeyote yule. Lakini ikihitajika kisheria kuhudhuria vikao vya korti, tunaweza hitajika kisheria kupeana maelezo yako ya kibinafsi. Si rahisi hili kufanyika, lakini linawezekana.

Hazina hii inaendeshwaje?

Ujumbe muhimu

Hazina hii inasimamiwa na mashirika ya jamii ya Washington yanayoongozwa na wahamiaji—watu wao hao ndio walioitisha kuundwa kwa hazina hii. Inaungwa mkono na kufadhiliwa na idara ya jamii na huduma za afya ya jimbo la Washington.

Ujumbe wa ziada

- Mashirika ya jamii yanayoongozwa na wahamiaji kote jimboni wanashirikiana na afisi ya Gavana, idara ya jamii na huduma za afya ya jimbo la Washington, na wakfu wa sheria ya Washington waliunda hazina hii. Wakati jimbo la Washington linatoa pesa na kufanya shughuli ya uangalizi, hawashughulikii na habari ya kibinafsi ya mtu.
- Mashirika ya jamii yanayosimamia hazina ndiyo yanayoweka vigezo, kushughulikia maombi ya watu, kusambaza pesa, na kuweka habari za kibinafsi za watu salama. Mashirika ya jamii yanayoongoza hazina hii ni:
    - Asian Counseling and Referral Service
    - Colectiva Legal del Pueblo
    - Fair Work Center
    - Legal Foundation of Washington
    - Northwest Immigrants Rights Project
    - Nuestra Casa
    - OneAmerica
    - Raiz of Planned Parenthood
    - Scholarship Junkies
    - Seattle Credit Union

    - Washington Census Alliance
    - Washington Dream Coalition
    - Washington Immigrant Solidarity Network
- Mashirika yote yanayohusika na hazina hii yamefanya kazi kwa miaka mingi na jamii za wahamiaji,ikiwa ni pamoja na wakulima wasiojiweza , wafanyakazi wenye mshahara mdogo, na wahamiaji weusi, wazawa, LGBTQIA2+, wanaoishi na ulemavu, na wengine wengi.Wote wamejitolea kwa ustawi na faragha ya jamii ya wahamiaji.

Je pesa kutoka kwa hazina hii inaweza nizuia nisipate visa au kadi ya kijani siku za usoni kwa sababu ya sheria ya malipo ya umma?

Ujumbe muhimu

Hapana. Usaidizi kutoka kwa hazina hii inachukuliwa kama msaada wa wakati mmoja kwa sababu ya janga na haitazingatiwa chini ya sheria ya malipo ya umma. Kupata usaidizi kutoka kwa hazina hakutaathiri uwezo wako wa kupata kadi ya kijani.

Zana za mawasiliano na vifaa

Tumia sampuli ya ujumbe ufuatao ili kusaidia kupitisha ujumbe kuhusu Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji katika jamii yako. Tafadhali kuwa huru kutengeneza ili zifae mashirika yako au sauti yako binafsi. Tunataka watu wengi iwezekanavyo ambao wanafuzu kwa hazina hii kutuma maombi. Hizi ni rasilimali zinazohitajika kwa haraka na tunataka kuhakikisha majirani wetu wahamaji na marafiki wanapata usaidizi na utunzaji unaostahili.

Hashitegi zinazopendekezwa

#WAImmigrantRelief
#WACOVIDRelief
#Coronavirus
#COVID19

Mfano wa chapisho la mtandao wa kijamii

Fesibuku

- Kama wahamiaji, tumefanya Washington kuwa nyumbani kwetu. Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia wakati mgumu kwa sababu ya COVID-19, na huwezipata msaada wa fedha ya serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira,Tuma maombi ya kupata Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji na upate dola elfu moja kama msaada wa fedha (hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba) inapatikana. Tuma maombi kwa: www.immigrantreliefwa.org.
- Maombi ya Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iko wazi kupokea maombi. Maelezo yako ya kibinafsi hayatasambazwa kwa hiari kwa serikali, ICE, na sheria ya malipo ya umma haipaswi kutumika katika hazina hii. Jifunze mengi na utume maombi kwa: www.immigrantreliefwa.org.
- Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iliundwa na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji. Maombi yako wazi kwa sababu ya msaada wa kifedha kwa wale walioathiriwa na COVID-19, wale wasioweza kupata msaada wa fedha za serikali au bima ya mtu asiyekuwa na kazi. Jifunze mengi na utume maombi kwa: www.immigrantreliefwa.org.
- Wahamiaji wanasaidiana. Tuma maombi sasa hivi kwa Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji, ni hazina mpya iliyoundwa kwa sababu ya wahamiaji walioathiriwa na tandavu ya virusi vya corona. Jifunze mengi na utume maombi kwa: www.immigrantreliefwa.org.

Twita

- Wahamiaji wanaosaidiana. Tuma maombi ili upate hazina hii mpya #WAImmigrantRelief Fund. Ikiwa wewe ni mhamiaji aliyeathiriwa na #COVID19, unawezafuzu kupata dola elfu moja kama msaada (na hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba). Jifunze mengi + tuma maombi sasa hivi kwa 1-844-724-3737 / www.immigrantreliefwa.org.
- Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji: na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji. Habari yako imelindwa + na haitawahi sambazwa kwa hiari kwa serikali au ICE, na sheria ya malipo ya umma haitatumika. Ikiwa wewe ni mhamiaji aliyeathiriwa na COVID-19, jifunze mengi kuhusu hazina hii na utume maombi sasa hivi. www.immigrantreliefwa.org.
- Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia hali ngumu kwa sababu ya COVID-19, na huwezipata msaada wa fedha za serikali au bima ya mtu asiyekuwa na kazi, tuma maombi kwa hazina #WAImmigrantRelief Fund. Hadi dola elfu moja kama msaada wa fedha (hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba) inapatikana. www.immigrantreliefwa.org
- Msaada wa dharura wa COVID-19 —na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji. Ikiwa wewe ni mhamiaji na huwezi kupata msaada wa serikali wa fedha au bima ya mtu asiyekuwa na kazi, tuma maombi kwa Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji sasa hivi na unawezapata hadi dola elfu moja kama msaada.$$. www.immigrantreliefwa.org

Instagramu

- Msaada wa dharura wa COVID-19 —na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji. Hazina hii mpya ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iliundwa ili kusaidia majirani wahamiaji na wafanyakazi walioathiriwa na COVID-19. Ikiwa wewe au mtu unayemjua anapitia wakati mgumu na huwezi pata msaada wa serikali wa fedha au bima ya mtu asiyekuwa na kazi, tuma maombi kwa hazina hii mpya ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji na upate hadi dola elfu moja kama msaada (na hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba). Jifunze mengi na utume maombi kwa www.immigrantreliefwa.org. #WAImmigrantRelief
- Kama wahamiaji, tumefanya Washington kuwa nyumbani kwetu. Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia wakati mgumu kwa sababu ya COVID-19, na huwezi pata msaada wa fedha wa serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira,Tuma maombi ya kupata Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji na upate dola elfu moja kama msaada (hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba) inapatikana. Habari yako imelindwa na haitasambazwa kwa hiari kwa serikali au ICE, na sheria ya malipo ya umma haitatumika. Tuma maombi kwa www.immigrantreliefwa.org #WAImmigrantRelief
- Wewe ni mhamiaji na unapitia hali ngumu kwa sababu ya #COVID19, na huwezi pata msaada wa fedha za serikali au bima ya mtu asiyekuwa na kazi? Hii ndio sababu tuliungana na mashirika mengine ya wahamiaji kote jimboni ili kuunda Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji. Sasa unaweza tuma maombi ili upate msaada wa pesa dola elfu moja (na hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba) kwa www.immigrantreliefwa.org. #WAImmigrantRelief

- Wahamiaji wanawasaidia wahamiaji. Hii ndiyo kazi ambayo hii hazina mpya ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iliundwa kufanya Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia hali ngumu kwa sababu ya COVID-19, na huwezipata msaada wa fedha za serikali au bima ya mtu asiyekuwa na kazi, tuma maombi sasa. Unaweza pata dola elfu moja kama msaada na hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba. Jifunze mengi kwa www.immigrantreliefwa.org. #WAImmigrantRelief

Jumbe fupi za kutumia machapisho ya picha (jumuisha nembo ya WIRF)

- Wahamiaji wanaotunzana
- Msaada wa dharura wa COVID-19 —na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji.
- Tuma maombi ili upate ufadhili wa COVID-19. tembelea www.immigrantreliefwa.org au piga simu kwa 1-844-724-3737.
- Ufadhili wa COVID-19 kwa wahamiaji. Salama na imelindwa.
- Tuma maombi sasa hivi.

Mfano wa nakala ya maandishi ya video

Tumia nakala ya maandishi ifuatayo kurekodi video yakujinasa ili isaidie kusambaza ujumbe kuhusu hazina hii na kuwahimiza watu kutuma maombi. Ni muhimu pia kuongeza upekee wako na sauti kwa video yako, Ipendekeza kwa nini wewe unafikiri hazina hii ni muhimu kwako wewe binafsi.

> *Kama wahamiaji,tumefanya nyumbani kwetu.*
>
> *Tunatia bidii kila siku ili kusaidia jamii yetu.*
>
> *Leo, na hii tandavu inayoathiri kila mtu karibu nasi, ni wakati wa kupata usaidizi unaostahili.*
>
> *Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iliundwa kwa sababu ya wahamiaji na wahamiaji hapa Washington ili kutoa msaada wa kifedha.*
>
> *Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia wakati mgumu kwa sababu ya COVID-19, na huna uwezo wa kupata pesa za serikali, hii hazina ni kwa ajili yako.*
>
> *Na unawezapata hadi dola elfu moja na hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba.maelezo yako yako salama.*
>
> *Tuma maombi kabla Disemba tarehe 6. Ili kufahamu mengi, tembelea www.immigrantreliefwa.org*
>
> *Sisi ni wahamiaji, na tunatunzana.*

Kama inawezekana, tunapendekeza uongeze slaidi mwishoni mwa video na uongeze nembo ya shirika lako na nembo WIRF.

Mfano wa arafa za simu

Jambo*[jina]*. Mimi ni *[jina lako]* kutoka *[shirika lako]*. Ni nataka kuhakikisha unafahamu kuhusu hazina mpya ya msaada kwa wahamiaji – iliyoanzishwa na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji ndani ya Washington.Ni ya wale watu ambao hawakufuzu kupata msaada wa serikali wa virusi vya corona kwa sababu ya hali zao za uhamiaji. Unapaswa kupata dola elfu moja ya kukusaidia wewe na familia yako. Jifunze mengi na utume maombi kwa www.immigrantreliefwa.org.

Jambo *[jina]*. Mimi ni *[jina lako]* kutoka *[shirika lako]*. Je ! umetuma maombi yako kwa Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji? Unaweza pata dola elfu moja kukusaidia wewe na familia yako wakati huu wa tandavu ya COVID-19. Nijuze iwapo una maswali, na ujifunze mengi au utume maombi kwa www.immigrantreliefwa.org.

Jambo *[jina]*. Mimi ni *[jina lako]* kutoka *[shirika lako]*. Bado unaweza tuma maombi kwa Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji.tuma maombi kwa www.immigrantreliefwa.org kabla Disemba tarehe before 6, na unaweza pata dola elfu moja kukusaidia wewe na familia yako.

Mfano wa yaliyomo katika barua pepe

Jambo *[jina], Mimi ni [jina lako] kutoka [shiirika lako].*

Kama wahamiaji tumefanya Washington nyumbani kwetu—na tunahitaji kusaidiana hapa wakati huu wa tandavu. Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji iliundwa na wahamiaji kwa sababu ya wahamiaji ili kuwapa msaada wa kifedha. Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia hali ngumu kwa sababu COVID-19, na haufuzu kupata msaada wa serikali wa kifedha au bima ya mtu asiyekuwa na kazi,hazina hii ni kwa ajili yako.

Tuma maombi kwa Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji na upate dola elfu moja utakayolipwa wakati mmoja na utatumiwa moja kwa moja (hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba).

Hazina hii iliundwa na mashirika ya jamii yanayoongozwa na wahamiaji *kama [shirika lako]*. Sisi *[au wao]* wanaendesha hazina na wanahusika na kushughulikia maombi ya watu na pesa, na hatuwezi kwa hiari sambaza habari yako kwa serikali au ICE,na sheria ya malipo ya umma haitatumika. Unaweza pata usaidizi unapotuma maombi kwa lugha kadhaa.

Tujuze ikiwa una maswali yoyote, jifunze mengi na utume maombi kwa www.immigrantreliefwa.org.